

JAMHURI YA MUUNGANO WA TANZANIA

BUNGE LA TANZANIA



ORODHA YA SHUGHULI ZA LEO

MKUTANO WA SABA

KIKAO CHA ISHIRINI NA MBILI

13 MEI, 2022



ORODHA YA SHUGHULI ZA LEO

MKUTANO WA SABA

KIKAO CHA ISHIRINI NA MBILI – TAREHE 13 MEI, 2022

I. DUA:

II. HATI ZA KUWASILISHA MEZANI:

WAZIRI WA AFYA:

Randama za Makadirio ya Mapato na Matumizi ya Wizara ya Afya kwa Mwaka wa Fedha 2022/2023.

III. MASWALI:

OFISI YA RAIS (TAMISEMI):

188. MHESHIMIWA GRACE VICTOR TENDEGA (VITI MAALUM):

Atamuuliza Mheshimiwa Waziri wa Nchi, Ofisi ya Rais (TAMISEMI):-

Je, ni vigezo gani vinapaswa vifuatwe na Halmashauri ili fedha za maendeleo ziweze kutolewa.

**189. MHESHIMIWA BENAYA LIUKA KAPINGA
(MBINGA VIJIJINI):**

Atamuuliza Mheshimiwa Waziri wa Nchi, Ofisi ya Rais (TAMISEMI):-

Je, ni lini Kituo cha Afya Mapera kilichopo Mbinga Vijijini kitaanza kutoa huduma ya mionzi na *Ultra Sound*.

**190. MHESHIMIWA JERRY WILLIAM SILAA
(UKONGA):**

Atamuuliza Mheshimiwa Waziri wa Nchi, Ofisi ya Rais (TAMISEMI):-

Je, Serikali haioni ni wakati muafaka wa kuwaingiza Wazee na Wanaume kwenye mikopo inayotolewa na Halmashauri.

WIZARA YA KILIMO:

**191. MHESHIMIWA KAVEJURU ELIADORY FELIX
(BUHIGWE):**

Atamuuliza Mheshimiwa Waziri wa Kilimo:-

Je, ni lini Serikali itakamilisha mchakato wa kuanza kilimo cha umwagiliaji katika Bonde la Mto Luiche Mkoani Kigoma.

WIZARA YA HABARI, MAWASILIANO NA TEKNOLOJIA YA HABARI:

192. MHESHIMIWA MARGARET SIMWANZA SITTA (URAMBO):

Atamuuliza Mheshimiwa Waziri wa Habari, Mawasiliano na Teknolojia ya Habari:-

Je, ni lini Serikali itajenga minara katika

- maeneo yasiyo na minara na kutatua matatizo ya mawasiliano katika maeneo yenye minara.

WIZARA YA MALIASILI NA UTALII:

193. MHESHIMIWA ERIC JAMES SHIGONGO (BUCHOSA):

Atamuuliza Mheshimiwa Waziri wa Maliasili na Utalii:-

Je, ni lini Serikali itazuia Mamba wanaoua watu na kujenga uzio wa nondo maeneo ambayo watu huchota maji Jimboni Buchosa.

194. MHESHIMIWA TUNZA ISSA MALAPO (VITI MAALUM):

Atamuuliza Mheshimiwa Waziri wa Maliasili na Utalii:-

Je, Serikali ina mkakati gani wa kukuza utalii wa Fukwe za Bahari nchini.

WIZARA YA UJENZI NA UCHUKUZI:

195. MHESHIMIWA YUSTINA ARCADIUS RAHHI (VITI MAALUM):

Atamuuliza Mheshimiwa Waziri wa Ujenzi na Uchukuzi:-

Je, ni lini barabara ya Dareda - Dongobesh, Katesh - Haydom, Karatu - Mbulu - Hydrom – Singida na Babati – Orkasmit itajengwa.

WIZARA YA AFYA:

196. MHESHIMIWA KABULA ENOCK SHITOBELA (VITI MAALUM):


Atamuuliza Mheshimiwa Waziri wa Afya:-

Je, Serikali ina mkakati gani wa kumaliza tatizo la Vifo vya Akinamama katika Mkoa wa Mwanza.

IV. HOJA ZA SERIKALI:

WAZIRI WA MAJI:

Kwamba, Bunge sasa likubali kupokea na kupitisha Makadirio ya Mapato na Matumizi ya Wizara ya Maji kwa Mwaka wa Fedha 2022/2023.



(Majadiliano yanaendelea)

**DODOMA
13 MEI, 2022**

**N.J. MWIHAMBI, *ndc*
KATIBU WA BUNGE**